# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA NANE

**5 FEBRUARI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA NANE – TAREHE 5 FEBRUARI, 2026

**I. DUA:**

**II. KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE:**

Mhe. Silyvestry Francis Koka

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

**127. MHESHIMIWA JOHN STEPHANO LUHENDE (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Shule ya Kidato cha Tano na Sita katika Jimbo la Bukene.

**128. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Mradi wa Bonde la Mto Msimbazi utaanza na kukamilika.

**129. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini ujenzi wa Soko la Mazao la Kimataifa katika eneo la Tacri Mbimba utaanza.

**130. MHESHIMIWA DEVOTHA DANIEL MBURARUGABA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali imeweka utaratibu gani kwa Vikundi vinavyopata Mikopo ya Halmashauri kupatiwa mafunzo ya usimamizi ili kuongeza ufanisi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**131. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (SAME MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka Wataalamu kwa Wakulima wa Tangawizi Tarafa ya Mamba Vunta na Gonja ili kuboresha umwagiliaji.

**132. MHESHIMIWA BARAKA ULIMBOKA MWAMENGO (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Miradi ya Umwagiliaji ya Mbuga ya Tenende na Katumba - Songwe itaanza.

**WIZARA YA NISHATI:**

**133. MHESHIMIWA SULEIMAN MOHAMED RASHID (MWERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia vyanzo vya Umeme vya Upepo na Jua vilivyopo nchini.

**134. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza usambazaji wa umeme kwenye Vitongoji vyote vilivyobaki Mkoani Kilimanjaro.

**WIZARA YA MAJI:**

**135. MHESHIMIWA ABDUL-AZIZ MOHAMED ABOOD (MOROGORO MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi mkubwa wa Maji wa Bilioni 185 utaanza Morogoro ikizingatiwa kuwa kuna kero kubwa ya maji.

**WIZARA YA UJENZI:**

**136. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, utaratibu gani wafuate Wananchi wanaofanya biashara pembezoni mwa Barabara za TANROADS hususan maeneo ya Mkambe, Kidatu na Mkula.

**IV. UCHAGUZI WA WAJUMBE KWENYE TAASISI MBALIMBALI:**

1. Tume ya Utumishi wa Bunge;
2. Wajumbe wa *(PAP)*;
3. Jukwaa la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC-PF)*;
4. Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)*; na
5. Umoja wa Maziwa Makuu *(Great Lakes)*.

## V. KAMATI YA MIPANGO:

### WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda mrefu 2026/27 - 2050/51, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/27.

### WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya 2026/27 - 2028/29.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **5 FEBRUARI, 2026** | **KATIBU WA BUNGE** |

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA